

Toleo la Julai, 2019

BARAZA LA MITIHANI LA TANZANIA

SR 2

FOMU YA UTHIBITISHO WA MATOKEO (STATEMENT OF RESULTS) UNAOKABIDHIWA KWA MTAHINIWA

A. UTANGULIZI

Kufuatia mahitaji na umuhimu wa kuwa na Uthibitisho wa Matokeo ambao mtahiniwa atakuwa nao muda wote na mahali popote utakapohitajika, Baraza la Mitihani la Tanzania limeamua kutoa Uthibitisho wa Matokeo utakaomilikiwa na mtahiniwa mwenyewe badala ya kuutuma moja kwa moja kwa Mamlaka ama Taasisi inayohitaji matokeo ya mtahiniwa husika. Huduma hii itatolewa kwa watahiniwa waliokuwa na **vyeti visivyo na picha.**

B. UTARATIBU WA MAOMBI

- (i) Toa taarifa ya upotevu wa cheti katika **Kituo cha Polisi.**
- (ii) Tangaza upotevu wa cheti kwenye Gazeti ukionesha **Jina la Mtahiniwa, Namba ya Mtihani, Aina ya Mtihani, Mwaka wa Mtihani, Jina la Shule, Picha ya Mtahiniwa** na **Mahali** cheti kilipopotea.
- (iii) Jaza fomu ya maombi na fanya malipo ya **Tshs. 100,000/=** na kisha ambatisha:-
 - Taarifa ya upotevu (**Police Loss Report**).
 - Ukurasa wa gazeti wenye tangazo la upotevu au barua ya Jeshi la Uokozi (**Fire Rescue Force**/serikali ya mtaa inayohusu kuungua/uharibifu.
 - Nakala ya Kitambulisho cha mpiga kura/taifa (uraia) au hati ya kusafiria (**Passport**) au leseni ya udereva. **Vitambulisho vingine havitapokewa.**
 - Picha Ndogo ya rangi (**Coloured Passport Size Photo**) yenye **“Blue background”** - Ibandikwe kwenye fomu.
- (iv) Wasilisha ombi lako la Uthibitisho wa Matokeo (**SR**) katika ofisi za NECTA au tuma kwa **Katibu Mtendaji**, Baraza la Mitihani la Tanzania, S.L.P 2624, Dar es Salaam au kwa njia ya barua pepe: esnecta@necta.go.tz.
- (v) Mchakato wa **uchunguzi** juu ya **uhalali** na **umiliki** wa taarifa za matokeo ya mtahiniwa na **uchapaji** wa Uthibitisho wa Matokeo (**SR**) **utakamilika** ndani ya **siku thelathini (30)** tangu kuwasilishwa kwa ombi la Uthibitisho huo wa Matokeo.
- (vi) Uthibitisho wa Matokeo (**SR**) **utatolewa** mara moja (**01**) tu.

C. UTARATIBU WA MALIPO

Malipo kwa ajili ya Uthibitisho wa Matokeo (**SR**) yafanyike kwa kutumia namba maalum (**Control Number**) inayotolewa na mfumo wa malipo ya serikali wa kielektroniki (**GePG**) kupitia tovuti ya **NECTA: www.necta.go.tz** au piga simu numba **+255-22-2700493...6** kwa msaada zaidi. Malipo yote yafanyike katika benki za: **-NMB; CRDB** na **NBC** au kwa kutumia mitandao ya kifedha ya **M-Pesa** na **TigoPesa.**

Toleo la Julai, 2019

BARAZA LA MITIHANI LA TANZANIA

SR 2

**FOMU YA UTHIBITISHO WA MATOKEO (STATEMENT OF RESULTS)
UNAOKABIDHIWA KWA MTAHINIWA**

PICHA NDOGO
YA
MTAHINIWA

D. TAARIFA ZA MTAHINIWA:

- (i) Jina kamili lililotumika katika mtihani
- (ii) Aina ya mtihani (CSEE, ACSEE, GATCE, GATSCCE, DEE/DSEE, GCE, FTC, ADE).....
- (iii) Mwaka wa mtihani
- (iv) Namba ya mtihani
- (v) Jina la Shule
- (vi) Anwani ya Mwombaji
- (vii) Simu
- (viii) Barua pepe.....
- (ix) Saini ya Mwombaji
- (x) Tarehe ya kuwasilisha fomu ya maombi

E. KWA MATUMIZI YA OFISI TU.

- (i) **Uthibitisho wa Malipo (Mhasibu)**
 - Kiasi cha fedha kilicholipwa **Tshs**.....
 - Namba ya Malipo (**Control Number**)
 - Jina la Mhasibu.....
 - Cheo.....
 - Saini ya Mhasibu.....
 - Tarehe.....
- (ii) **Uthibitisho wa Kupokea Fomu ya Maombi (Afisa - Chumba Namba 15)**

Nakiri kupokea ombi la SR likiwa na viambatisho vyote tajwa hapo juu;
Jina la Afisa aliyepokea fomu ya maombi.....
Saini.....
Tarehe
- (iii) **ICRD - Ombi limeshughulikiwa/halijashughulikiwa kwa sababu**
 - (a)
 - (b)
 - (c)

Jina la Afisa aliyeshughulikia.....
Saini

Tarehe